**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA MKOA MBEYA.**

**S. L. P 320, KYELA – MBEYA.**

---

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA MKOA MBEYA,

S. L. P 320,

**KYELA - MBEYA.**

25/10 / 2024

**SIMU: 1. MKUU WA SHULE: 0754 668 190**

**2. MAKAMU MKUU WA SHULE: 0756 660 505**

**3. MWALIMU WA MALEZI: 0759 374 737**

Mzazi wa ______________________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MBEYA (MBEYA GIRLS SECONDARY SCHOOL) MWAKA 2025.**

1. Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya wasichana ya Mbeya **“**Mbeya Girls**”** iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

   Muhula wa masomo utaanza tarehe 13**. 01. 2025** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **13. 01. 2025 .**

2. **MAHALI SHULE ILIPO.**

   Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa **“**Mbeya girls**”** ipo Mkoani Mbeya Wilaya ya Kyela, Kata ya Busale.

   **“NAMNA YA KUFIKA”.**

   - Kwa wale wanaotokea Mbeya, panda magari yanayoenda Kyela , Ipinda au Matema, shukia kituo kinaitwa **SIMSOKWE** kituo hiki kipo kabla ya kufika junction ya Boda. Ukifika hapo utaona kibao cha shule kinaonyesha shule ilipo waweza chukua usafiri maarufu kwa Jina la Bodaboda au unaweza kutembea toka Barabara Kuu panaumbali takribani Km 1 tu.
   - Na kwa wale wanaotokea Barabara ya Kyela au Boda Kituo **SIMSOKWE** kipo baada ya Junction ya Boda.

**3. NAULI**

Kwa mabasi ya Abiria toka Mbeya nauli ni elfu saba tu (Tsh.7,000/= )

Na Kutoka Kyela au Boda Nauli ni Elfumbili tu ( Tsh. 2,000/= ) .

- Bodaboda toka barabarani mpaka shuleni ni Elfu moja tu ( Tsh. 1,000/= )

**4. SARE YA SHULE.**

4.1 wakati wote wa muda wa masomo mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni :-

i. Sketi 2, moja iwe rangi ya ( Dark Gray ) kijivu nyeusi ndefu mpaka kisigino , Rinda box kubwa mbele na nyuma na ya pili draft kubwa yenye mchanganyiko wa rangi, kama inavyo onekana kwenye picha hapo chini.

ii. Kwa Waislamu waje na Hijabu 2 nyeupe na mashati 2 mikono mirefu.

iii. Mashati 2 meupe ya mikono mifupi.

iv. Neck Tai ya rangi ya sketi ( dark Gray ) kijivu nyeusi.

v. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu.

vi. Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu jozi mbili.

vii. T-shirt mbili rangi ya dark blue zenye nembo ya shule ( Hizo utazikuta shuleni kwa bei ya Tsh. 15,000/= )

viii. Tracksuit moja rangi dark blue yenye ufito mweupe.

ix. Gauni ( Shamba dress ) rangi ya maruni. Mshono wa solo ndefu mpaka kisigino mikono izidi kidogo kiwiko.

x. Jezi rangi ya blue iliyokolea na T- shirt yake zisiwe na urembo mwingi. (Bukta iwe pana)

xi. Raba Nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo.

xii. Sweta rangi ya kijivu nyeusi ( Rangi ya sketi ) yenye **“ v ”**



**DRAFTI**



**KIJIVU NYEUSI ( DARK GRAY)**

**5. MAHITAJI MENGINE.**

**i.** Aje na Godoro moja futi mbili na nusu na shuka 4 rangi ya pinki iliyokolea au **waweza nunulia hapahapa shuleni kwa bei zifuatazo:-**

1. Godoro futi 2½ Tsh. 35,000/= , 2. Shuka Tsh.10,000/= @1

- ❖ **MWANAFUNZI ASIJE NA BLANKETI KWANI HALI YA HEWA NI JOTO MWAKA MZIMA.**

ii. Chandarua cha duara cheupe.
iii. Soksi nyeusi ndefu za kujikinga na mbu wakati wa jioni.
iv. Ndoo ndogo mbili kwa matumizi yake binafsi.
v. Vyombo vya kulia chakula ( sahani , kijiko na kikombe )
vi. Ndala au yebo za kuogea.
vii. Viatu vya wazi ( sendozi ) nyeusi . Hivi atavaa baada ya muda wa Masomo na siku za weekend.
viii. Karatasi (Ream) A4 nyeupe mbili. Moja kila muhula.
ix. Daftari kaunta ( Q3 ) 10 na madogo aina ya msomi 10 .
x. Peni rangi ya blue, Pencil, rula na mkebe wenye vifaa vyote.
xi. File 02 aina ya plastiki.
xii. Picha mbili ( Passport size ) utapiga shuleni kurahisisha utengenezaji wa vitambulisho. Gharama yake haizidi 5,000/=
xiii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
xiv. Nguo za ndani zisizopungua 6, Taiti 3 na doti ya kanga , taulo 01 , sabuni za kufulia , kuogea na Mafuta ya kupaka ya kawaida.
xv. Aje na sanduku la chuma. ( Tranka ) Kwaajili ya kutunzia vitu vyake.

- ➢ **KWA SABABU YOYOTE HARUHUSIWI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI**.

**6. SHERIA ZA SHULE.**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya Mwaka 1978.Pia inazingatia Miongozo yote Inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Hivyo kwa kipindi chote utakapo kuwa mwanafunzi wa shule hii utatakiwa kushika na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule ukiwa ndani na nje ya shule.

**A. TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE.**

i. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele kwa kipindi chote atakachokuwa ukisoma hapa.

**ii. HESHIMA:**

- kila mwanafunzi anatakiwa kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu walimu, Wazazi / walezi , Wageni ,viongozi na wanafunzi wenzie kwa ujumla na kuzingatia Usafi binafsi.

iii. **MAWASILIANO:**

- Kiingereza ndiyo lugha pekee ya mawasiliano hapa shuleni. Hivyo mwanafunzi haruhusiwi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote isipokuwa tu wakati wa midahalo ya Kiswahili.

iv. **RATIBA YA SHULE.**

- Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu Ratiba ya shule . Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya Mazingira ya shule bila ruhusa maalumu kutoka kwa Uongozi wa shule.
- Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na kutii wito ( kengere )

**B. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE.**

i. Wizi wa aina yoyote.

ii. Uwasherati, Ushoga, Usagaji.

iii. Ulevi wa pombe, Matumizi ya madawa ya kulevya kama vile:- Bangi , Mirungi na Kuberi n . k

iv. Kupiga/kupigana / kutukana/ kutoa lugha chafu kwa wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla.

v. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.

vi. Kudharau Bendera ya Taifa.

vii. Kubeba Mimba/ kutoa mimba.

viii. Kugoma/Kuchochea, kuongoza mgomo na Kuvuruga Amani na Usalama shuleni/ Jamii.

ix. Kumiliki simu/ Line / Charger/ Memory card/ Flash au kifaa chochote kinachohusiana na simu ikiwemo **“Smartwatch”**

x. Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani yote.

xi. Kugomea adhabu yoyote halali.

xii. Kuto tii Serikali iliyopo Madarakani na Chama Tawala.

xiii. Kuwa nje ya shule bila Sare ya shule na bila ruhusa / kibali maalumu kutoka kwa Uongozi wa shule.

xiv. Kuonekana kwenye nyumba za wageni na kumbi za starehe.

xv. Utoro/ kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini ( 90 ) bila taarifa.

- **MAKOSA YAFUATAYO YAKIJIRUDIA YANAWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI.**
    i. Kuchelewa kufika shuleni baada ya likizo.
    ii. Kutovaa Sare rasmi ya shule kulingana na Ratiba ya shule.
    iii. Uchafu wa mwili. ( kutonyoa nywele , kutooga n . k ) na kutokutunza miundombinu na mazingira ya Shule.
- **ANGALIZO.**
    - Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vifaa vya Umeme kama vile Pasi, Heater n . k. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kumiliki Tv, Redio awapo mazingira ya shule.
    - Kwa kuwa mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu au laini , Shule imeweka Utaratibu . Mawasiliano yote yapitie kwa mwalimu wa Malezi namba yake ni :**0759 374 737** na Mwalimu wa Nidhamu namba yake ni: **0753 468 391** na si vinginevyo.
    - Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vitu vyenye ncha kali kama vile:- **Visu, Bisibisi, mkasi, sindano, Nyembe n . k**
    - Mwanafunzi asije na **mafuta makali, Marashi, na aina zote za perfume, sabuni zenye kemikali hatarishi.**
    - **Mapambo kama mikufu , Hereni, cheni , Vikuku , Bangili, n . k HAVIRUHUSIWI**
- **Mwanafunzi aje na Bima ya Afya.**
    - **Kama hana Bima aje na Fedha kiasi cha Tsh. 10,000/= kwa ajili ya kukata bima ya ICHF ( Improved Community Health Fund )**
- **Shule haitoi huduma ya mlo maalumu wa kujitegemea (Special diet)**

***"HONGERA SANA KWA KUCHAGULIWA, KARIBU SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA MKOA( MBEYA GIRLS)".***

GWILA. G. KASEBELE
MKUU WA SHULE.
0754 668 190

HEADMISTRESS
MBEYA GIRL'S SEC. SCHOOL
KYELA

**KIAMBATISHO (A )**

**FOMU YA KUKUBALI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA.**

**SHULE YA SEKONDARI MBEYA GIRLS.**

---

Mimi ______________________________ Mwanafunzi bila shuruti nakubali kutumia nafasi niliyopewa ya kidato cha ____________________ katika Shule ya sekondari ya Wasichana Mbeya. Pia nimesoma na kuelewa maelekezo yote yaliyomo katika fomu hii, naahidi kuyazingatia yote ikiwa ni pamoja na kutoshiriki kwa namna yoyote ile katika tabia zozote za utovu wa nidhamu.

Saini____________________

Mwanafunzi.

Mimi ______________________________ mzazi / mlezi wa ______________________________( mwanafunzi ) . Nimesoma masharti yote yaliyomo katika fomu ya Mwanangu ya kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa Mbeya girls, ninakubali na kuahidi kwamba nitawajibika sawasawa kwa jambo lolote linalomhusu mwanangu . Aidha nitakuwa tayari kushirikiana na Uongozi wa Shule kuhakikisha mwanangu anamaliza Elimu ya kidato cha nne.

Saini ______________________

Mzazi/ Mlezi

**KIAMBATISHO ( A )**

**FOMU YA KUKUBALI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA.**

**SHULE YA SEKONDARI MBEYA GIRLS.**

---

**MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.**

1. Jina kamili( Majina matatu kama yalivyo kwenye matokeo ya darasa la saba)

   ______________________________________________________________

2. A) Tarehe ya kuzaliwa______________________________

   B) Mahali alipozaliwa ______________________________

3. Dini ______________________________ Dhehebu ______________________
4. Uraia _____________________________
5. Kama siyo Raia wa Tanzania taja Uraia wako ________________________
6. Shule ya Msingi uliyotoka ____________________________________
7. A). jina kamili la Mzazi / Mlezi _______________________________________

   B). Anwani ya Mzazi / Mlezi ________________________________________

   C). Kazi ya Mzazi / Mlezi ____________________________________________

   D) Kituochake cha Kazi _____________________________________________

   E ) Namba ya Simu __________________________________________________

   F ) Jina la Mwenyekiti wa Mtaa / Kitongoji ___________________________

   Namba yake ya Simu _____________________________________________

**ATTACHMENT ( C )**

**KYELA DISTRICT COUNCIL.**

**MBEYA GIRLS SECONDARY SCHOOL.**

**P. O . BOX 320, KYELA - MBEYA**

DATE: ______________________

**RE: REQUEST MEDICAL EXAMINATION**

MEDICAL OFFICER IN CHARGE,

______________________________

______________________________

STUDENT'S NAME: __________________________________________________________

Please examine the above named students as to the physical / mental fitness/ Unfitness for admission as full – time student of Mbeya Girls secondary school for academic year 2024/ 2025.

The examination should include the following categories.

Eye sight, Hearing, Epilepsy,Urine, Venereal disease, Stool and any other body deformation.

THE HEADMISTRESS,

MBEYA GIRLS SECONDARY SCHOOL,

P. O. BOX 320,

KYELA – MBEYA.

**RE: MEDICAL EXAMINATION RESULTS**

I have examine the above student and found her with the following disease/ Impairment/ disabilities.

Eye Sight……………………………………………………………………………………………………..

Urine examination ……………………………………………………………………………………………

Hearing ……………………………………………………………………………………………………...

Stool examination ……………………………………………………………………………………………

Speech ………………………………………………………………………………………………………

Venereal disease …………………………………………………………………………………………..

Limbs …………………………………………………………………………………………………………

Epilepsy ……………………………………………………………………………………………………..

Pregnancy test…………………………………………………………………………………………….

Additional Information / Other serious diseases …………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………..

Medical remarks ……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

Name and signature of attending Officer ……………………………………………………………………

Date ………………………………………. Official Stamp…………………………………………..........................